**KISWAHILI**
**KIDATO CHA NNE**
**MUHULA 3 2025**

# Mwongozo wa Kusahihisha

**Maswali**
Eleza sababu za watu kuweka pesa kwenye benki. (ala 1)
- **Ili kuondokewa na wasiwasi kwani wanafahamu fedha zao ziko salama.**

b) Fafanua hatari za kuweka fedha au kuficha nyumbani au kuzichimbia chini. (ala 3)
- **Zinaweza kuibiwa na wezi**
- **Zinaweza kutumiwa ovyo ovyo kwa sababu zipo**
- **Huenda zikapotea**
- **Zinaweza kuharibiwa na mchwa**
- **Zinaweza kutoweka ikiwa nyumba inaharibiwa na moto au mafuriko**
- **Zinaweza kuozea humo mwenyewe akifa bila kuacha wasia wowote.**

**(zozote 3)**

c) Eleza faida ya kulipa deni kwa kutumia hundi. (ala 2)
- **Unapunguza hatari ya wizi**
- **Unarahisisha malipo kwa watu wanaoishi mbali.**

d) Eleza faida anazopata mtu anayeweka pesa zake kwenye benki. (ala 2)
- **Anaweza kupata riba ilipwayo kila mwaka hivyo pesa yako huongezeka.**
- **Anaweza kulipa madeni yake kwa hundi.**

e) Eleza maana ya msamiati kama ulivyotumika katika kifungu.
Akiba
- **Fedha inayowekwa ili itumike baadaye**

f) Andika methali yenye maana sawa na ujumbe unaowasilishwa katika kifungu hiki. (ala 1)
- **Akiba haiozi**

**Matumizi ya lugha (alama 30)**
a) Toa sauti zifuatazo ukizingatia uzuiliaji wa hewa. (ala 2)
i) /ny/
- **Ni king'ong'o/ kipua/ nazali**

ii) /y/
- **Ni kiyeyusho**

b) Tunga sentensi ukitumia kitenzi –ja katika kauli ya kutendewa. (ala 2)
**- ja – (Jiwa) – Mtoto alijiwa na mzazi shuleni (mwalimu akadirie jibu sahihi)**

c) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo. (ala 3)
**aliwafurahisha**

**A - li - wa - furahi - sh - a**

- **A** – **Nafsi**
- **li** – **wakati**
- **wa** – **kitendewa**
- **furahi** – **mzizi**
- **sh** – **kauli**
- **a** – **kiishio**

d) Weka shadda katika maneno haya. (ala 2)


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

i) Mbio - **'Mbio**
ii) Samawati - **sama'wati**
e) Changanua sentensi kwa njia ya jedwali. (ala 4)
Yeye aliupita mtihani huo ingawa alikuwa mgonjwa.

| **S** | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **SI** | | | | **U** | **S2** | | |
| **KN** | **KT** | | | | **KN** | **KT** | |
| **W** | **T** | **N** | **V** | | | **t** | **N** |
| **Yeye** | **aliupita** | **mtihani** | **huo** | **ingawa** | **Q** | **Alikuwa** | **mgonjwa** |

f) Andika katika usemi halisi. (ala 3)
Mama alituahidi kuwa angetununulia zawadi kama tungekamilisha kazi aliyokuwa ametupa.
**"Nitawapa zawadi kama mtakamilisha kazi ambayo nimewapa," mama alituahidi.**
g) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo. (ala 3)
Waandamanaji wengi walikusanyika kando ya barabara leo asubuhi.
**Kirai nomino – waandamanaji wengi**
**Kirai kihusishi – kando ya barabara**
**Kirai kitenzi – walikusanyika kando ya**
**Kirai kielezi – leo asubuhi.**
**(zozote 3)**
**(mwanafunzi asiandike kirai cha neno moja)**

h) Tunga sentensi moja kutofautisha vitate vifuatavyo. (al 2)
Vaa na faa
**Wakati wa joto unafaa kuvaa nguo nyepesi**
**(mwalimu akadirie majibu ya mwanafunzi)**
i) Bainisha matumizi ya neno kijinga katika sentensi;
kitoto kijinga kilichomwa kwa kijinga. (ala 2)

↓ **kivumishi** ↓ **Nomino**

j) Eleza tofauti zilizo kwenye sentensi zifuatazo. (ala 2)
i) Kazi yoyote itafanywa na mafundi hawa.
**Bila kuchagua/ kutojali/ kutobagua**
ii) Kazi yote itafanywa na mafundi hawa.
**Kwa ujumla au bila kubakisha**
k) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (al 2)
KN (N+V+V) + KT (t + N)
**Mtoto yule mdogo alikuwa mgonjwa.**
**Mtoto yule mchanga angali mgonjwa**
**Mwanariadha huyo hodaru alikuwa Mkenya.**
**(mwalimu akadirie majibu ya mwanafunzi.**
l) Bainisha shamrisho katika sentensi ifuatayo.
Nyanya atapandiwa mbegu kwa panga ya mjomba. (ala 3)
**Nyanya – shamrisho kitondo**
**Mbegu – shamrisho kipozi**
**Panga ya mjomba – shamrisho ala**

**ISIMU JAMII (ALAMA 5)**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

"Haya basi, beba mmoja! Beba mmoja. Dada njoo! Nafasi ni ya mmoja. Ni mbao tu. Bei ya chini kuliko keki. Usiachwe antie, bei ni poa."

a) Tambua sajili inayorejelewa na maneno haya. (ala 1)

**Biashara ya usafiri barabarani**

b) Fafanua sifa nne za sajili hiyo. (ala 4)

- **Sentensi huwa fupi mf; Baba, beba, dada njoo!**
- **Lugha sio sanifu mf; Ni mbao tu**
- **Kuna kuchanganya ndimi; Town, driver, change**
- **Lugha yenye msamiati maalum; Beba, lipa, pesa**
- **Lugha ya utohozi hutumika mf. Steji, dereva, petroli**

**FASIHI SIMULIZI (ALAMA 5)**

Fafanua istilahi zifuatazo.

i) Soga
**Mazungumzo ya kupitisha wakati**

ii) Mawaidha
**Mazungumzo ya kutoa ushauri/ kuelekeza**

iii) Misimu
**Maneno au misemo inayozuka kwa kipindi fulani kisha hutoweka baada ya muda**

iv) Lakabu
**Majina ya kupanga yanayopewa mtu/ watu kutokana na sifa, tabia au maumbile**

v) Maapizo

- **Maombi maalum yanayofanywa kwa Mungu, miungu au mizimu ili kumtaka mtu aliyetenda dhambi kulaaniwa**
- **Kumwombea laana mtu aliyetenda uovu.**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke